

## Maswali

1. Mbona Stephano alipigwa mawe?
2. Nani alishuhudia?
3. Sauli alitaka kufanyaje wanafunzi?
4. Sauli aliona na kusikia nini alipokuwa akienda Dameski?
5. Sauti ilisema nini?
6. Sauli alijihisi namna gani?
7. Mbona Sauli aliongozwa kwenda Dameski?
8. Mwanafunzi yupi alienda kuona Sauli?
9. Hakutaka kwenda, mbona?
10. Aliambia Sauli nini?
11. Sauli alifanya nini kwanza?
12. Nini ingesaidia Sauli kwa kazi yake ya kufundisha?
13. Ni nini ya maana tunayo fundishwa na Sauli?

## Majibu

1. Kwa kufundisha kwamba Yesu ni mwana wa Mungu
2. Sauli
3. Kuwarudisha Yerusalemu na awaue
4. Mwangaza mkubwa kutoka mbinguni.
5. “Sauli, Sauli, mbona unafanya kazi kinyume na mimi?”
6. Alitishika sana
7. Alikuwa amepofuka
8. Anania
9. Alikuwa amesikia kwamba Sauli ako kinyume ya wafuasi wa Yesu.
10. Yesu alimwambia amwendee Sauli kwa sababu alikuwa amechaguliwa kuhubiria Wayunani, wafalme na watu wa Israeli.
11. Alibatizwa.
12. Roho Mtakatifu
13. Kwamba Yesu ni mwana wa Mungu

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

# 49 Sauli anaenda Dameski

## Marejeo

Matendo ya mitume 7:57-60; 8:1; 9:1—19

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu huchagua yeyote anayetaka amfanyie kazi


## Maneno maalum

1. Stephano + piga mawe + Sauli + Dameski.
2. Mwangaza mkubwa + sauti + tisha
3. Watu waogopa + hakuona + ongozwa + siku tatu.
4. Anania + maono + endea Sauli + chagua
5. Wekea mkono + ona tena + fikiria na kuomba
6. Magamba + ona + kazi ya kufanya + habari njema
7. Batizwa + funza + hubiri + kazi ikaanza

**49.1** Wanafunzi hawakukuwa na wakati mzuri wakuhubiri kila siku. Stephano mfwasi wa Yesu alipigwa mawe na akafa kwa sababu ya kufundisha kwamba Yesu ni mwana wa Mungu. Sauli aliangalia wakimpiga mawe. Alitaka wafwasi wengi wa Yesu wafe iwesekanavyo. Wanafunzi wengi walitoroka Yerusalemu kwa sababu ya vitisho. Sauli aliamua kwenda Dameski kuwafuata. Alienda kuwarudisha wote Yerusalemu waume na wake.

**49.2** Aliposafiri kwenda Dameski alizuiliwa na mwangaza mkubwa. Mwangaza ulitoka mbinguni. Sauli alianguka jini. Akasikia sauti, “Sauli, Sauli, mbona unafanya kazi kinyume changu?”

Sauli aliuliza, “Unani wewe Bwana?” Sauti ilimjibu, “Mimi ni Yesu. Unafanya kazi kinyume changu.” Sauli alikuwa akitetemeka mwili wote. Alitishika sana. “Unataka nifanye nini?” Yesu alisema, “Simama enda Dameski utaambiwa cha kufanya kule.”



**49.3** Watu waliokuwa na Sauli waliogopa pia. Walikuwa wakisikia sauti lakini hawakuona ye yote. Sauli alisimama. Akafungua macho lakini hangeweza kuona. Walimshika mkono na kumwongoza hadi Dameski.

Sauli alikusudia kufika Dameski kwa sauti, akitisha wanafunzi. Badala yake aliongozwa kwa ajili hakukuwa anaona. Aliogopa na hakuweza kula wala kunywa kwa siku tatu. Aliomba Mungu amsaidie.

**49.4** Anania, mwanafunzi wa Yesu aliishi Dameski. Katika maono Mungu alimwambia aende amuone Sauli. Anania hakutaka kwenda. “Nimesikia kwamba Sauli amefanya kazi kinyume na Yesu, kwanza Yerusalemu na sasa Dameski.” Malaika alisema, “Enda kwa sababu nimemchagua Sauli kuhubiria Wayunani, wafalme na watu wa Israeli.”

**49.5** Anania alienda kuona Sauli. Lazima alikuwa na wasiwasi. Aliingia kwa nyumba na kuweka mikono yake juu ya Sauli. Akasema, “Ndugu Sauli, nimetumwa na Mungu. Utaona tena. Utapewa nguvu ya Roho mtakatifu ya kukusaidia ufundishe.”

Sauli alikuwa akiwaza na kuomba. Alijua kilichofanyika kwa Yesu. Vile alikufa na vile Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Sasa alifahamu kwamba Yesu alikuwa mwana wa Mungu!

**49.6** Magamba yalipotoka kwa macho yake – angeona! Angeona kwa sababu alikuwa na kazi ya kufanyia Mungu. Mungu alikuwa amemchagua aeneze habari njema ya Yesu kwa mataifa yote ya milki ya Rumi.

**49.7** Kwanza, alibatizwa. Alionyesha kwamba ameamini na kuelewa habari ya injili. Alikaa kwa muda huko Dameski pamoja na wanafunzi. Lakini baadhi yao hawakumpenda, akatoroka kwa kuteremshwa juu ya ukuta ndani ya kikapu. Baadaye alianza kufundisha katika hekalu. Akihubiri, “Yesu ni mwana wa Mungu.” Kazi yake kwa Mungu ilikuwa imeanza.

